Je Hekalu Lako Linahitaji Kusafishwa?

na

Ellis P. Forsman

Je Hekalu Lako Linahitaji Kusafishwa?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Je Hekalu Lako Linahitaji Kusafishwa?

Matt. 21:12-14

Muda mfupi baada ya kuingia Yerusalemu mwanzo wa wiki yake ya mwisho, Yesu aliingia hekaluni.

Math. 21:12-14, "*Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akapindua meza za wabadili fedha na viti vyao walivyokuwa wakiuza njiwa; akawaambia Imeandikwa nyumba yangu itaitwa Nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. Na vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni akawaponya.*"

Aliuthiwa na uwepo wa wale wabadilisha fedha na wafanya biashara, aliwatoa nje. Akawahuzunikia kwa kugeuza nyumba ya Mungu kuwa pango la wanyang'anyi. Pamoja na hekalu kusafishwa pia aliwaponya vipofu na viwete.

Kabla ya hapo tayari Yesu alikuwa ameshasafisha hekalu.

Yoh. 2:13-17, "*Na Pasaka ya Wayahudi ilikuwa karibu, naye Yesu akakwea mpaka Yerusalemu. Akaona pale hekaluni watu waliokuwa wakiuza ng'ombe na kondoo na njiwa, na wenye kuvunja fedha wameketi. Akafanya kikoto cha kambaa, akawatoa wote katika hekalu, na kondoo na ng'ombe; akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akapindua meza zao; akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa, yaondoeni haya; msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara. Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa imeandikwa, Wivu wa nyumba yako utanila.*"

Ilikuwa ni wakati wa Pasaka, miaka mitatu kabla.

Alafu akawakemea kwa kuigeuza nyumba ya Mungu kuwa nyumba ya biashara.

Katika matukio hya yote, tunaona hasira ya Yesu kwa kutumia vibaya hekalu; sio kwamba kulikuwa na ubaya katika ununuzi na uuzaji, bali haikuwa sehemu sahihi, au matumizi ya hekalu.

Vipi kuhusu hekalu lako? Je linatumika kwa njia sahihi? Je linahitaji kusafishwa? Unatambua kwamba unahekalu?

Ndiyo, unahekalu. Kama ilivyo kwa hekalu la Yerusalemu, inapaswa itumike katika huduma na kumsifu Mungu. Kama sio, basi na lenyewe linahitaji kusafishwa! Je naongea kuhusu nini?

Mwili wako ni hekalu

Ni hekalu ambalo Mungu anakaa ndani yake.

Mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu, ni nani aliyeko ndani yako kama wewe ni Mkristo. 1 Kor. 6:19, "*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe.*"

"*Ukaaji huu*" unaonyesha uhusiano wa kipekee kati yako na Roho Mtakatifu.

Ambayo Mungu anakutia nguvu.

Efe. 3:16, "*Awajalie kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*"

Kupitia kwake tunaweza kushughulikia uwezo wa dhambi.

Rum. 8:11-13, "*Lakini, ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu. Basi, kama ni hivyo ndugu, tu wadeni, si wa mwili tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.*"

Kama Suleimani alivyotambuliwa na hekalu kule Yerusalemu, hakuna uwepo wa kimwili unaoweza kuwa na uwepo wa kila mahali wa Mungu; hiyo ni, Mungu ambaye yupo kila mahali kwa wakati mmoja.

2 Nyakati. 6:18, "*Lakini Mungu je yamkini atakaa na watu dunia? Tazama mbingu na mbingu za mbingu za mbingu hazikutoshi; siuze nyumba hii niliyoijenga.*"

Hiyo ni kweli hata kwa Roho wa Mungu.

Zaburi 139:7-12, "*Niende wapi nijiepushe na roho yako? Kama ningepanda mbinguni Wewe uko; ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko. Ningezitwaa mbawa za asubuhi, na kukaa pande za mwisho za bahari; huko nako mkono wako utaniongoza, na mkono wako wa kuume utanishika. Kama nikisema hakika giza litanifunika, na nuru inizungukayo ingekuwa usiku; giza nalo halikufichi kitu, basi usiku huangaza kama mchana; giza na mwanga kwako ni sawasawa.*"

Jehanamu – Kiebrania ni "Sheol" katika mustari huu – ni sehemu ya kusubiria ya nafsi baada ya mtu kufa katika maisha haya.

Vile vile, upekee wa uwepo wa Roho katika maisha ya Mkristo ni muhimu kiasi kwamba ni sahihi kuiongelea "*ukaaji*" Mkristo. Gal. 4:6,

"*Kwa sababu ninyi ni wana, Mungu ametuma Roho ya Mwanaye katika mioyo yenu, aliaye, Aba, yaani Baba.*"

Kile ambacho kinasemwa kuhusu mwili wa damu na nyama pia inasemwa kuhusu kanisa kwa ujumla.

1 Kor. 3:16, "*Hamfahamu ya kuwa ninyi ni hekalu la Mungu, na kwamba Roho wa Mungu hukaa ndani yenu?"*

Paulo alikuwa anazungumza kuhusu kanisa katika mistari inayoendelea:

1 Kor. 3:9-15, "*Maana sisi tu wafanyakazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jingo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie anavyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo. Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itadhihirishwa, kwa kuwa yafunuliwa kwa moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gain. Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata thawabu. Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto.*"

Kinachosemwa kuhusu kanisa kama hekalu pia ni kweli kuhusu mwili. 1 Kor. 3:17, "*Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo; kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.*"

Chafua hekalu la Mungu na utakumbana ghadhabu ya Mungu! Kwa kuwa hekalu linapaswa kuwa takatifu! Tunahekalu ambalo linatakiwa lijitoe kwa ajili ya kumhudumia Mungu.

Hekalu la Yerusalemu lilipaswa kuwa sehemu ya sala.

- Math.21:13, "*Akawaambia, imeandikwa, nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.*"
- 2 Nyakati. 6:19-21, "*Walakini umwangalie mtumwa wako anayoyaomba, nakushi ee BWANA, Mungu wangu usikie kilio na maombi anayoyaomba mtumwa wako mbele zako; ili macho yako yafumbuke kwa nyumba hii mchana na usiku mahali uliponena, ndipo utakapoliweka jina lako; usikie maombi atakayoomba mtumwa wako akikabili mahali hapa. Uyasikie atakayosihi mtumwa wako, na watu wako Israeli, watakapoomba wakikabili mahali hapa; naama, usikie toka makaoni mwako, toka mbinguni nawe usikiapo samehe.*"

Hivyo, hekalu lako, ikijumlisha mwili na akili, lazima zijitoe katika huduma kwa Mungu. Mwili wako unapaswa uwe dhabihu iliyohai.

- Rumi.12:1, "*Nawasihi ndugu zangu kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyohai, takatifu, inayokubaliwa na Mungu, ndiyo ibaada yenu ya maana.*"
- Wakol. 3:5-9, "*Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tama mbaya, mawazo mabaya, na kutamani ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake.*"

Nia yako lazima ifanywe upya, itazame vitu vilivyoko juu.

- Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"
- Wakol. 3:1-2, "*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.*"

Tusiruhusu hekalu la Mungu lichafuliwe. Tumeona jinsi hekalu la Yerusalemu lilivyo chafuliwa. Sehemu iliyopendekezwa kwa ajili ya sala, iligeuzwa kuwa soko. Sehemu ambayo iliitajika kasafishwa, mara moja na tena.

Hii inaweza kuwa kweli kuhusu hekalu letu. Tunaweza kuwa na hatia kwa kuweka mawazo yetu katika vitu vya dunia. Tunaanza kutumikia matumbo yetu (ladha ya kimwili), badala ya Yesu.

Fil.3:18-19, "*Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani.*"

Tunajikuta sisi wenyewe hatuwezi kukaa katika mapenzi ya Mungu.

Rum. 8:5-8, "*Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.*"

Tunaanza kuruhusu hekalu la Mungu lichafuke kwa kutoa miili yetu mahali ambapo haipaswi kuwa. Baadhi ambayo kimsingi ni dhambi.

1 Kor. 6:13-18, "*Vyakula ni vya tumbo, na tumbo ni kwa vyakula; lakini Mungu atavitowesha vyote viwili, tumbo na vyakula. Lakini mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili. Naye Mungu alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake. Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha! Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, wale wawili watakuwa mwili mmoja. Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye. Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.*"

Vitu vingine (kujali, utajiri, starehe ya maisha) ambayo utuondoa katika huduma yetu ya kweli na kubana uwezo wetu wa kumtumikia Mungu kwa miili yetu.

Luka 8:14, "*Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lolote.*"

Hali ya hekalu lako ikoje? Labda upo katika hitaji la "furaha kuu" (wokovu). Labda upo katika hitaji la "kusafishwa" (kurejeshwa na kuwekwa wakifu). Katika shauri lo lote, mifumo ya kusafishwa ni dhahiri.

Unahitaji nini ili uweze kusafishwa – uwepo wa Kristo

Yesu ni mzoefu katika "kusafisha hekalu"! Hata zaidi, inapokuja wakati wa kusafisha hekalu ya miili yetu na roho zetu. Anafahamu kwamba inapaswa kuanzia ndani nje.

Math. 23:25-27, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. Ewe Farisayo kipofu, safisha kwanza ndani ya kikombe, ili nje yake nayo ipate kuwa safi. Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi.*"

Yesu alikufa ili aweze kututakasa.

Tito 2:11-14, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitumainia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa*

Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema."

Damu yake ndio uwezo unao safisha inatutakasa kutoka katika dhambi zote.

1 Yoh. 1:7, *"Kama tukitembea nuruni, kama yeye alivyonuruni, tuna ushirika sisi kwa sisi na damu ya Yesu Kristo mwanaye hutusafisha na dhambi zote.*"

Hiyo ndio zawadi yake kwetu.

Tunahakikishaje uwepo wa Kristo katika "hekalu" zetu?

Kupitia imani.

Efe. 3:17, "*Ili Kristo aweze kukaa katika mioyo yenu kwa imani, ili muweze kusimama imara kwa upendo.*"

Tunapaswa kuwa na imani itendayo kazi. Yakobo 2:18-20, "*Lakini mtu asema, wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani kwa njia ya matendo yangu. Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vyema. Mashetani nao waamini na kutetemeka. Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?*"

Kupitia utii.

- Yoh. 14:21, "*Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*"
- Yoh. 14:23, "*Yesu akajibu akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.*"
- 1 Pet. 1:22, "*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.*"

Kwa asiye Mkristo, imani hii na utii inajumuisha ubatizo.

Ubatizo unatuunganisha na Kristo ili kwamba mwili wa dhambi uweze kufa.

Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka*

katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."

Katika ubatizo tunamvaa Kristo. Wagal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo Yesu mmemvaa Kristo.*"

Kupitia ubatizo Mungu, Roho Mtakatifu, na Yesu Kristo wanaingia katika miili yetu. Miili yetu inakua hekalu ya wote watatu.

Kwa Mkristo aliye na hitaji la kusafishwa, imani ya utii inajumuisha toba na sala.

Matendo. 8:22, "*Basi tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikira hii ya moyo wako.*"

Toba inahitajika, kama Kristo alivyotoa ushauri kwa Walaodokia.

Ufu. 3:14-19, "*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika; haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Nayajua matendo yako ya kuwa hu baridi wa hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi kwa sababu una uvugu vugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kintwa changu. Kwa kuwa wasema, mimi ni tajiri, nimejitajirisha wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako upate kuona. Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii ukatubu.*"

Badili mambo unayoyafanya. Badili tabia.

Sala inahitajika kwa kile ambacho Bwana anaruhusiwa katika mioyo yetu. Ufu. 3:20, "*Tazama nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.*"

Tunamfikia kwa maombi.

Unahitaji uwe na nini ili uweze kusafishwa – uwezo wa Kristo

Yesu alionyesha nguvu kwa kugeuza meza na kuwafukuza wafanya biashara nje; hata zaidi sana, anatoa nguvu kwa ajili ya Wakristo.

Pasipo yeye, hatuwezi kufanya chochote.

Yoh. 15:4-5, "*Kaeni ndani yangu nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa pekee yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hmwezi kufanya neno lo lote. "*

Pamoja naye, tunayaweza mambo yote kupitia yeye.

Wafil. 4:13, "*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*"

Hiyo ni, tunaweza kufanya chochote kulingana na mapenzi yake. Hiyo ndio maana tuna Roho Mtakatifu; kutusaidia wakati tunapokutana na magumu.

Hivyo, tunapaswa kusimama imara.

Efe. 6:10, "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake.*"

Usiwe Mkristo wa uvuguvugu. Simama imara.

- Wakol. 1:11, "Mkiwezeshwa na uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha;"
- Isa. 41:10, "*Usiogope kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike kwa maana mimi ni Mungu wako, nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.*"

Unahitaji uwe na nini ili uweze kusafishwa – kushiriki pamoja na Kristo.

Wakati tegemeo letu lipo kwa Kristo kwa ajili ya kusafishwa, hatuwezi kukaa tu. Lazima tuchukue hatua ya "kujisafisha wenyewe".

2 Kor. 7:1, "*Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.*"

Tuache kufanya vitu na miili yetu ambavyo Bwana anavichukia. Lazima "tuwe na utakatifu". Ebr. 12:14, "*Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nayo;*"

Hii inajumuisha vyote "kuvua" na "kuvaa" vitu katika maisha yetu.

Kama Yakobo alivyo shauri.

Yak. 1:21, "*Kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu.*"

Kama Petro alivyofundisha.

1 Pet. 2:1-2, "*Basi wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote. Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu;*"

Kama Paulo alivyoamuru.

Efe. 4:22-32, "*Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tama zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho na nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha mwenzake. Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe ibilisi nafasi. Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema lenye kufaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*"

Kusafishwa kwetu kutastawishwa na kile tunachoruhusu katika akili zetu. Kwa maana vitu vinavyofaa kutukuzwa na wema utahakikisha uwepo wa Mungu katika maisha yetu.

Fil. 4:8-9, "*Hatimaye ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo. Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi."*

Kugeuzwa kwetu kutatokea wakati ambapo nia zetu zinafanywa upya.

Rum. 12:1-2, "*Basi ndugu zangu nawasihi, kwa huruma zake Mungu itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"

Hitimisho

Hekalu lako lipo katika hali gain? Je ni sehemu ambayo Mungu, Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu wanaweza kukaa?

Je mwili na akili yako ni "sehemu ya maombi"; ambazo huleta utukufu kwa Mungu? Au umeyaruhusu vitu vichafu ya maisha haya kukaa katika hekalu lako kitu ambacho Mungu hakukusudia, kwamba ni sehemu najisi na chafu?

Kama hekalu lako linahitaji kusafishwa, basi mtazame Yesu. Anaweza tu kutoa utakaso unaouhitaji. Pia anatoa uwezo wa kuishi kiungu.

Lakini kuwa makini kwamba usimuruhusu Yesu kusafisha hekalu lako na si chochote. Kwa sababu kusafishwa pasipo mbadala inaweza kuharibu mambo.

Math. 12:43-45, "*Pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzikia asipate. Halafu, husema, nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka hata akija aiona tupu, imefagiwa na kupambwa. Mara huenda akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kilicho kibaya.*"

Hivyo, tunapaswa kujaza hekalu letu kwa maombi, sifa, wema, na uungu. Vinginevyo hekalu zetu zitzjaa na sanamu.

Usisahau maneno ya Mtume Paulo:

2 Kor. 6:16-7:1, "*Tena pana mapatano gain kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema ya kwamba, nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami*

nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo tokeni kati yao mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana mwenyezi. Basi wapenzi wangu kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu."

Je unashirikiana na Kristo katika usafishaji na kukamilisha utakatifu katika kumuogopa Mungu?